

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA.



WILAYA YA KALAMBO

**TAARIFA YA WILAYA YA KALAMBO KWA MHE. KASSIM MAJALIWA
MAJALIWA (MB) WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA WAKATI WA ZIARA YAKE WILAYANI KALAMBO
TAREHE 24 AGOSTI, 2016.**

MKUU WA WILAYA (W),
KALAMBO,
S.L.P 1,
MATAI.

AGOSTI, 2016

YALIYOMO

1	UTANGULIZI	1
1.1	Utawala	1
1.2	Muundo wa baraza la madiwani la Halmashauri.....	1
1.3	Idadi ya watu.....	1
1.4	Ukubwa wa eneo la Wilaya.....	2
1.5	Shughuli za kiuchumi	2
1.6	Hali ya ulinzi na usalama.....	2
2	TAARIFA YA UKUSANYAJI WA MAPATO	3
2.1	Matumizi ya kieletroniki katika ukusanyaji wa mapato.....	3
3	SEKTA YA UTAWALA NA UTUMISHI	4
3.1	Utambuzi wa watumishi hewa.....	4
3.2	Hatua zilizochukuliwa baada ya zoezi la uhakiki.....	4
3.3	Mikakati ya kuondoa tatizo la watumishi hewa	5
3.4	Utambuzi wa watumishi wenyewe vyeti feki.....	6
4	SEKTA YA ELIMU MSINGI	6
4.1	Uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya awali.....	6
4.2	Uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza	7
4.3	Maendeleo ya taaluma	7
4.4	Maendeleo ya taaluma kwa darasa la nne (IV).....	8
4.5	Maendeleo ya taaluma kwa darasa la saba (VII)	8
4.6	Elimu ya watu wazima.....	8
4.7	Miundombinu ya shule kwa ujumla.....	8
4.8	Uhakiki wa wanafunzi hewa	9
5	SEKTA YA ELIMU SEKONDARI	9
5.1	Hali ya walimu.....	9
5.2	Udahili wa wanafunzi kidato cha kwanza mwaka, 2016.....	9
5.3	Hali ya taaluma kidato cha pili (FTSEE)	10
5.4	Hali ya taaluma kidato cha nne (CSEE)	10
5.5	Hali ya taaluma kidato cha sita (ACSEE).....	10
5.6	Taarifa ya ujenzi wa maabara	10
5.7	Miundombinu ya shule kwa ujumla.....	11

5.8	Taarifa ya mapokezi ya wanafunzi wa kidato cha tano.....	11
6	TAARIFA YA MADAWATI.	13
6.1	Mikakati wa kukamilisha matenegenezo ya madawati.....	13
6.2	Elimu bila malipo.....	14
7	TAARIFA YA UTOAJI HUDUMA ZA AFYA	15
7.1	Hali ya watumishi na utumishi katika sekta ya afya	15
7.2	Miundombinu, samani na vifaa vya usafiri katika idara ya afya.....	16
7.3	Magonjwa kumi (10) yanayoathiri zaidi wananchi	17
7.4	Huduma za chanjo ya mama na mtoto.....	17
7.5	Mafanikio katika utoaji wa huduma za afya.	18
8	USAIFI WA MAZINGIRA	20
9	SEKTA YA MAJI	20
9.1	Upatikanaji wa huduma ya maji	20
10	SEKTA YA UJENZI	21
10.1	Utekelezaji wa miradi ya ujenzi	22
10.2	Miradi ya mwaka wa fedha 2015/2016	22
10.3	Mapokezi ya fedha.....	22
11	TAARIFA YA UJENZI WA NYUMBA ZA VIONGOZI WAANDAMIZI WA WILAYA 23	
11.1	Taarifa ya mradi wa nyumba za viongozi katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kalambo.	23
11.2	Taarifa ya ujenzi wa nyumba saba za watumishi wa Halmashauri	23
12	SEKTA YA KILIMO	24
12.1	Hali ya chakula msimu wa mwaka 2015/16.....	25
12.2	Mfumo wa utoaji wa pembejeo za ruzuku 2015/2016.....	25
12.3	Changamoto za mfumo wa utoaji pembejeo	28
12.4	Mipango inayolenga kuleta matokeo makubwa (BRN)	28
12.5	Maandalizi ya ununuzi wa mahindi kuitia NFRA.....	29
12.6	Kuanzisha uzalishaji wa zao wa kahawa	29
12.7	Kuanzisha uzalishaji wa zao la ufuta	30
12.8	Kilimo cha umwagiliaji.	30
12.9	Hali ya vyama vya ushirika	31
13	SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI	31
13.1	Idadi ya mifugo na wafugaji.	32
13.2	Huduma za mifugo	32
13.3	Soko la mifugo.....	32

13.4 Hali ya miundombinu.....	32
13.5 Migogoro baina ya wafugaji na wakulima	33
14 SEKTA YA UVUVI.....	33
14.1 Vyombo vya uvuvi.....	33
14.2 Miundombinu ya uvuvi	34
15 SEKTA YA ARDHI.....	34
15.1 Upimaji wa viwanja na vijiji.....	34
15.2 Utoaji wa hati miliki.	34
15.3 Mpango wa uandaaji wa ‘Master Plan’ ya miji yetu.....	35
15.4 Ulipaji wa fidia kwenye maeneo yaliyofanyiwa uthamini.	35
15.5 Mpango wa matumizi bora ya ardhi.....	35
15.6 Migogoro ya ardhi na utatuzi wake.	35
16 SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII.....	36
16.1 Mpango wa kunusuru kaya maskini – TASAF	36
16.2 Taarifa dhidi ya mapambano ya UKIMWI	36
17 SEKTA YA NYUKI	37
18 SEKTA YA SHERIA	38
19 SEKTA YA TEHAMA.....	39
20 HALI YA UWEKEZAJI WILAYANI NA FURSA ZA UWEKEZAJI ZILIZOPO	40
21 CHANGAMOTO, MIKAKATI NA UTATUZI WA CHANGAMOTO	41
22 HITIMISHO	43

MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Hali halisi ya makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kipindi cha 2013/2014, 2014/2015 na 2015/16.....	3
Jedwali Na. 2: Hali ya watumishi Wilaya ya Kalambo	4
Jedwali Na. 3: Hali ya uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali	7
Jedwali Na. 4: Hali ya uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza kwa kipindi cha miaka mitatu.....	7
Jedwali Na. 5: Hali ya taaluma kwa darasa la nne katika kipindi cha miaka mitatu.....	8
Jedwali Na. 6: Hali ya taaluma kwa darasa la saba katika kipindi cha miaka mitatu	8
Jedwali Na. 7: Hali halisi ya miundombinu ya shule na samani	8
Jedwali Na. 8: Hali ya walimu	9
Jedwali Na. 9: Udhili wa wanafunzi kidato cha kwanza.....	9
Jedwali Na. 10: Hali ya Miundombinu na samani katika idara ya Elimu Sekondari....	11
Jedwali Na. 11: Mapokezi ya wanafunzi kidato cha tano	12
Jedwali Na. 12: Miundombinu katika shule za sekondari.....	12
Jedwali Na. 13: Takwimu za madawati.....	13
Jedwali Na. 14: Hali halisi ya Watumishi katika Sekta ya Afya	15
Jedwali Na. 15: Hali ya Miundombinu,samani na vifaa vya usafiri.....	16
Jedwali Na. 16: Idadi wagojwa wa nje na ndani.....	17
Jedwali Na. 17: Chanjo zitolewazo na idadi ya walengwa	18
Jedwali Na. 18: Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi	22
Jedwali Na. 19: Mgawanyo wa vocha za pembejeo zilizogawiwa kwenye ngazi ya kata na idadi ya vocha zilizotumika.....	26
Jedwali Na. 20: Ukarabati wa wa Maghala tisa (9)	28
Jedwali Na. 21: Maandalizi ya ununuzi wa mahindi kupitia NFRA.....	29
Jedwali Na. 22: Hali ya skimu za Umwagiliaji	30
Jedwali Na. 23: Hali ya miundombinu katika sekta ya Mifugo na Uvuvi.....	33
Jedwali Na. 24: Maeneo yaliyopimwa viwanja.....	34
Jedwali Na. 25: Orodha ya fursa zilizopo katika Wilaya ya Kalambo.....	40
Jedwali Na. 26: Orodha ya wawekezaji waliopo katika Wilaya ya Kalambo.....	40

VIFUPISHO

AEHO	Assistance Environment Health Officer
AMCOS	Agriculture Marketing Cooperative Society
AMO	Assistance Medical Officer
ANO	Assistance Nurse Officer
BRN	Big Results Now
CBPP	Bovince Contagious Prepneumonia
CCM	Chama Cha Mapinduzi
CHADEMA	Chama cha Demokrasia na Maendeleo
CHF	Community Health Fund
CO/CA	Clinical Officer
CSEE	Certificate Secondary Education Examination
DADPs	District Agriculture Development Programmes
EHO	Environment Health Officer
EN	Enlorid Nurse
FBOs	Faith Based Organizations
FMD	Foot and Mouth Disease
FTSEE	Full Technical Secondary Education Examination
H/ASS	Health Assistance
HCMIS-LAWSON	Human Central Management Information System
HLAB TECH	Health Laboratory Technologist
LAB/ASS	Laboratory Assistance
LAN	Local Area Network
LGRCIS	Local Government Revenue Collection and Information System
MATT	Medical Attendant

MD	Medical Doctor
MVIWATA	Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania
NCD	New cattle Disease
NFRA	National Food Reserve Agency
NHIF	National Health Insurance Fund
NO	Nurse Officer
OC	Other Charges
PCCB	Preventing and Combating Corruption Bureau
POS	Point Of Sale
SACCOS	Saving and credit cooperative society
TACRI	Tanzania Agriculture Certifying Research Institute
OR - TAMISEMI	Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali Za Mitaa
TTCL	Tanzania Telecommunication Company Limited
U.T.I	Urinary Tract Infections
VEO	Village Executive Officer
WARC	Ward Agriculture Resource Centre
WEO	Ward Executive Officer

**TAARIFA YA WILAYA YA KALAMBO KWA MHE. KASSIM MAJALIWA
MAJALIWA (MB) WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA WAKATI WA ZIARA YAKE WILAYANI KALAMBO**
TAREHE 24 AGOSTI, 2016

1 UTANGULIZI

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Kalambo, napenda kukukaribisha katika Wilaya ya Kalambo na tunatoa shukrani zetu za dhati kwa uamuzi wako wa kuja katika Wilaya ya Kalambo.

Wilaya ya Kalambo ilianzishwa rasmi Julai 01, 2012 kwa tangazo la Serikali (GN 72) na Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ilianzishwa tarehe 23 Desemba, 2012 kwa kumegwa toka Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na kutangazwa kuwa Halmashauri Mwezi Januari 2013 kwa tangazo la Serikali (GN 631). Halmashauri ilianza kutekeleza Bajeti yake rasmi kuanzia tarehe 01 Julai 2013.

1.1 Utawala

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Makao Makuu ya Wilaya yapo katika Mji wa Matai umbali wa kilometra 52 kutoka Makao ya Mkoa wa Rukwa. Wilaya hii ina Jimbo 1 la Uchaguzi, Tarafa 5, Kata 23, vijiji 111 na vitongoji 439.

1.2 Muundo wa baraza la madiwani la Halmashauri

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Baraza la Madiwani lina wajumbe 32 akiwemo na Mhe. Mbunge. Kati ya hao, wajumbe waliochaguliwa ni 24 na Viti maalumu 8. Chama cha mapinduzi (CCM) kina wajumbe 23 na Chama cha Demokrasia na maendeleo (CHADEMA) wajumbe 9.

1.3 Idadi ya watu

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Wilaya ya Kalambo ina watu 207,700 kati yao Wanaume wapo 100,474 na Wanawake wapo 107,226. Kwa mwaka huu 2016 Wilaya hii

inakadiriwa kuwa na watu 238,760 ambapo wanawake wanakadiriwa kuwa 123,261 na wanaume 115,499.

1.4 Ukubwa wa eneo la Wilaya

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo ina eneo la kilometa za mraba 4,715. Kati ya hizo kilometa za mraba 504 ni za maji na kilometa za mraba 4,211 ni za nchi kavu.

1.5 Shughuli za kiuchumi

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Uchumi wa Wilaya ya Kalambo unategemea zaidi kilimo ambacho kinaajiri zaidi ya asilimia 90 ya wakazi wote wa Wilaya hii na kiasi kinachobaki ni Uvuvi, Ufugaji na biashara ndogondogo. Mazao yanayolimwa ni Mahindi, Alizeti, Maherage, Ulezi, Ngano, Karanga, Muhogo, Mtama na Viazi. Ziada ya Mazao haya ya chakula hutumika kwa biashara. Aidha shughuli za ufügaji, uvuvi, urinaji asali na biashara ndogondogo ni ajira mbadala zinazochangia katika pato la wakazi wa Wilaya ya Kalambo.

1.6 Hali ya ulinzi na usalama

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo ina vituo 4 vya polisi ambapo kituo 1 kipo katika Kata ya Matai (Makao Makuu ya Taraifa ya Matai), kituo cha 2 kipo katika Kata ya Kasanga (Makao Makuu ya Taraifa ya Kasanga), kituo cha 3 kipo katika Kata ya Mwimbi (Makao Makuu ya Taraifa ya Mwimbi), na kituo cha 4 kipo mpakani mwa Tanzania na nchi jirani ya Zambia katika Kijiji cha Kasesya.

Matukio machache ya uvunjifu wa amani ambayo yamekuwa yakidhibitiwa kwa wakati na vyombo vya dola kwa kushirikiana na wananchi wazalendo/raia wema kupitia dhana ya ulinzi shirikishi na polisi jamii. Pia hali ya mpaka na nchi jirani za Zambia na Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC) ni shwari.

2 TAARIFA YA UKUSANYAJI WA MAPATO

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo kupitia Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2015/2016 imekusanya jumla ya Tshs.1,163,144,064.59 ikiwa sawa na asilimia 82.08 ya mapato ya ndani. Kati ya fedha hizo, shilingi 527,440,548.59 ni makusanyo ya Halmashauri kwa Bajeti ya mwaka 2015/16, shilingi 635,703,516.00 ni deni la ushuru wa mahindi toka kwa wakala wa Taifa wa hifadhi ya chakula (NFRA) kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na 2014/2015.

Jedwali Na. 1: Hali halisi ya makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kipindi cha 2013/2014, 2014/2015 na 2015/16

Mwaka	Makadirio	Makusanyo	% ya makusanyo
2013/2014	872,241,500.00	742,809,000.00	85.16
2014/2015	1,023,611,000.00	822,334,648.89	80.33
2015/2016	1,416,973,000.00	1,163,144,064.59	82.08

Chanzo: *Idara ya Fedha, Julai 2016.*

2.1 Matumizi ya kieletroniki katika ukusanyaji wa mapato

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo inakusanya mapato yake ya ndani kwa njia ya kawaida kwa kutumia Watendaji wa Kata na Vijiji kupitia stakabadhi za Halmashauri (HW5) kutokana na changamoto ya kutokuwepo mawasiliano ya Mkongo wa Taifa. Aidha tarehe 12/07/2016 mtaalamu kutoka kampuni ya VSAT Africa kwa niaba ya TTCL alikuja kufanya utafiti wa mahali ambapo panafaa kuweka dishi la V-SAT kwa ajili ya mawasiliano ya intaneti kama ambavyo TTCL wameagizwa na TAMISEMI ili kufanikisha zoezi la Halmashauri kuunganishwa katika mifumo mbalimbali ikiwamo Epicor na mfumo wa kukusanya mapato (LGRCIS). Ufungaji wa dishi unaendelea katika eneo la Idara ya fedha. Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo tayari ina kompyuta mbili (2) kwa ajili ya ukusanyaji mapato kwa njia ya kieletroniki.

3 SEKTA YA UTAWALA NA UTUMISHI

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo ina uhitaji wa watumishi 3217. Waliopo Halmashauri ni 2060 (Asilimia 65) na Ofisi ya Katibu Tawala (W) ni 17 (Asilimia 39), hivyo kufanya upungufu kuwa watumishi 1140 (Asilimia 35) kati ya watumishi 3217 kama inavyoonekana katika majedwali hapa chini.

Jedwali Na. 2: Hali ya watumishi Wilaya ya Kalambo

Watumishi	Mahitaji	Waliopo	% Waliopo	Pungufu	% Pungufu
Halmashauri	3173	2060	65	1113	35
Ofisi ya Katibu Tawala (W)	44	17	39	27	61
Jumla	3217	2077	65	1140	35

Chanzo: *Idara ya Utawala na Utumishi na Ofisi ya Katibu Tawala (W), Agosti, 2016*

3.1 Utambuzi wa watumishi hewa

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Baada ya agizo la mwezi Machi, 2016 lilitolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kutambua, kuondoa na kuwachukulia hatua za kisheria watumishi hewa wote, Wilaya Kalambo iliripoti mtumishi hewa mmoja. Baada ya kuendelea na zoezi la uhakiki kwa kina Wilaya ya Kalambo ilibaini watumishi hewa 13 hadi kufikia April, 2016.

Hata hivyo, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa aliagiza lifanyike zoezi la utambuzi wa wafanyakazi hewa kwa kuhakiki orodha za mishahara kwa watumishi waliolipwa isivyo halali kuanzia Julai, 2013 hadi Mei, 2016, baada ya zoezi hilo watumishi 37 walibainikia kuchukua fedha iliyo na thamani ya shilingi 385,402,300/= isivyo halali.

3.2 Hatua zilizochukuliwa baada ya zoezi la uhakiki

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo imechukua hatua zifuatazo baada ya zoezi la uhakiki wa wafanyakazi hewa;

- i. Baada ya uchambuzi huo wa kina serikali ya Mkoa iliagiza zoezi la urejeshaji fedha lianze mara moja. ukiondoa fedha ambazo mishashara yake iliwekwa zuio benki, Wilaya ya Kalambo imefanikiwa kurejesha kiasi cha fedha Tshs. 13,000,000/= jitihada za kurejesha zinaendelea kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali kama vile Polisi na PCCB.
- ii. Baadhi ya wakuu wa Idara, wakuu wa vituo vya Afya na Zahanati na wakuu wa shule wameandikiwa barua zikiwataka kujiyeza kwa kosa la kushindwa kutoa taarifa mapema za watumishi watoro, waliofariki, waliocha kazi na wagonjwa wa muda mrefu hali iliyopelekea kusababisha hasara kwa Serikali.

3.3 Mikakati ya kuondoa tatizo la watumishi hewa

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo imeandaa mikakati mbalimbali ili kuondoa tatizo la watumishi hewa kama inavyoainishwa hapa chini;

- i. Halmashauri imeimarisha mfumo wake wa utoaji taarifa kwa watumishi watoro, waliofikisha umri wa kustaafu, wagonjwa wa muda mrefu, wanaohama, wanaoacha kazi na wanaofariki.
- ii. Kila Mkuu wa Idara anakabidhiwa orodha ya majina ya watumishi yaliyotolewa kwenye mfumo wa HCMIS – LAWSON na kukiri watumishi wanaostahili na wasio stahili kulipwa kila mwezi.
- iii. Kuzuia hundi za wastaafu waliochukua fedha za serikali zilizozidi pasipo kustahili
- iv. Kuweka zuio la mshahara wa mtumishi katika benki mara taarifa ya utoro wa mtumishi inapotolewa kwa mwajiri toka kwenye kituo chake chake cha kazi
- v. Kupitia orodha ya malipo ya serikali kuanzia tarehe 25 mpaka tarehe 4 ya kila mwezi na kuwaondoa katika orodha ya malipo ya Serikali watumishi wanaostaafu, wanaoacha kazi na wanaofariki kwa kushirikiana kwa karibu na Wakuu wa Idara husika.

vi. Kuhakiki orodha ya uhamisho wa watumishi inayotolewa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kujiridhisha na uhamisho wa watumishi kabla ya kuanza utaratibu wa kuwahamisha. `

3.4 Utambuzi wa watumishi wenye vyeti feki.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Sambamba na zoezi la uhakiki wa watumishi hewa, Wilaya ya Kalambo inaendelea na utambuzi wa watumishi wenye vyeti feki, hadi kufikia Julai, 2016 imebaini watumishi wanne (4) wenye vyeti feki na kumi na tatu (13) vyenye utata. Watumishi wanne (4) ni wa Idara ya Afya ambao wamefikishwa mahakamani, pia vyeti vya watumishi 13 vyenye utata vimepelekwa Baraza la mitihani na baraza la waugazi kwa ukaguzi.

4 SEKTA YA ELIMU MSINGI

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo ina jumla ya shule za msingi 98 ambazo ni za Serikali zenyne idadi ya wanafunzi 56,868 wakiwemo wavulana 28,364 na wasichana 28,504. Idadi ya walimu wanaohitajika ni 1,264, waliopo ni 978 (sawa na asilimia 77.37 ya mahitaji) kati yao wanaume ni 684 na wanawake 294, upungufu ni walimu 286 (sawa na asilimia 22.63 ya mahitaji). Aidha Wilaya ina jumla ya waratibu Elimu kata 23 na Maafisa wa Elimu ni 9.

4.1 Uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya awali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo ina madarasa ya awali katika shule zote za msingi, idadi ya wanafunzi wa madarasa ya awali ni 10,315 wakiwemo wavulana 5190 na wasichana 5125.

Jedwali Na. 3: Hali ya uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali

Mwaka	Waliotarajiwa			Walioandishwa			% Ya Uandikishaji
	Wat	Was	Jumla	Wat	Was	Jumla	
2014	3812	3261	7073	3456	3149	6605	93.4
2015	3580	3917	7497	3623	3822	7445	99.3
2016	3682	3594	7276	5190	5125	10315	141.8

Chanzo: Idara ya Elimu msingi, Julai 2016.

4.2 Uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo imeandikisha jumla ya wanafunzi wa darasa la kwanza 13,075 kati yao wavulana ni 6,719 na wasichana ni 6,356.

Jedwali Na. 4: Hali ya uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mwaka	Waliotarajiwa			Walioandikishwa			% ya uandikishaji
	Wat	Was	Jumla	Wat	Was	Jumla	
2014	5749	5692	11441	4703	4718	9,421	82.3
2015	4736	5210	9946	4641	4671	9,312	93.6
2016	4561	4149	8,710	6719	6356	13,075	150.1

Chanzo: Idara ya Elimu msingi, Julai 2016

4.3 Maendeleo ya taaluma

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Maendeleo ya Taaluma katika Wilaya ya Kalambo yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka kwa darasa la nne (IV) na darasa la saba (VII). Mchanganuo wa maendeleo ya Taaluma kwa darasa la nne na darasa la saba kwa kipindi cha miaka mitatu (3) ni kama inavyoonekana katika majedwali yafuatayo.

4.4 Maendeleo ya taaluma kwa darasa la nne (IV)

Jedwali Na. 5: Hali ya taaluma kwa darasa la nne katika kipindi cha miaka mitatu

Mwaka	Waliosajiliwa			Waliofanya			Waliofaulu			% Ya Ufaulu
	Wav	Was	Jum	Wav	Was	Jum	Wav	Was	Jum	
2013	2,828	2,783	5,611	2,292	2,396	4,688	1,526	1,328	2,854	61
2014	2,410	2,427	4,837	2,146	2,221	4,367	1,086	924	2,010	46
2015	2,294	2,484	4,778	2,055	2,314	4,369	1,535	1,543	3,078	69.58

Chanzo: Idara ya Elimu msingi, Julai 2016

4.5 Maendeleo ya taaluma kwa darasa la saba (VII)

Jedwali Na. 6: Hali ya taaluma kwa darasa la saba katika kipindi cha miaka mitatu

Mwaka	Waliosajiliwa			Waliofanya			Waliofaulu			% Ya Ufaulu
	Wav	Was	Jum	Wav	Was	Jum	Wav	Was	Jum	
2013	2,108	2,197	4,305	1,959	2,072	4,031	680	340	1,020	25
2014	1,923	2,084	4,007	1,840	2,010	3,850	724	419	1,143	30
2015	1,767	1,915	3,682	1,703	1,868	3,571	834	592	1,426	39.9

Chanzo: Idara ya Elimu msingi, Julai 2016

4.6 Elimu ya watu wazima.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo ina vituo kumi na tatu (13) vya Elimu nje ya mfumo rasmi vyenye idadi ya wanafunzi 335 wakiwemo wanaume 185 na wanawake 150. Idadi ya vituo vya ufundu ni 2, ambavyo ni Mwazye na Matai vyenye jumla ya wanafunzi 82 kati yao wavulana 43 na wasichana 39.

4.7 Miundombinu ya shule kwa ujumla

Jedwali Na. 7: Hali halisi ya miundombinu ya shule na samani

Miundombinu na samani	Mahitaji	Iliyopo	Asilimia (%)	Upungufu	Asilimia(%)
Madarasa	1,264	638	50.5	626	49.5
Nyumba za walimu	1,264	546	43.2	718	56.8
Matundu ya vyoo	2,563	1058	41.3	1,505	58.7
Meza	2,150	862	40.1	1,288	59.9

Chanzo: Idara ya Elimu msingi, Julai 2016

4.8 Uhakiki wa wanafunzi hewa

Wilaya ya Kalambo imeendelea kutekeleza agizo la Serikali la kuwabaini wanafunzi hewa. Idadi ya wanafunzi hewa waliobainika ni 921, kati yao wavulana ni 559 na wasichana ni 362. Zoezi la kuhakiki wanafunzi hewa linaendelea.

5 SEKTA YA ELIMU SEKONDARI

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ina Jumla ya shule za sekondari 19 kati ya shule hizo shule 15 zinamilikiwa na Serikali na shule 4 ni za binafsi. Shule za sekondari za bweni zinazomilikiwa na Serikali ni mbili zenyenye kidato cha tano na sita ambazo ni Mambwe na Matai. Wilaya ya Kalambo ina jumla ya wanafunzi 4,391 wa Sekondari kwa shule za serikali wakiwemo wavulana 2,696 na wasichana 1,695. Shule za binafsi zina wanafunzi 492 ambapo wavulana ni 279 na wasichana ni 213.

5.1 Hali ya walimu

Jedwali Na. 8: Hali ya walimu

Walimu	Mahitaji	waliopo	% Uwepo	Upungufu	% Upungufu
Masomo ya Sanaa	277	225	81	52	19
Masomo ya Sayansi	223	42	19	181	81
Jumla	500	267	53	233	47

Chanzo: Idara ya Elimu sekondari Julai, 2016.

5.2 Udhili wa wanafunzi kidato cha kwanza mwaka, 2016.

Udhili wa wanafunzi wa kidato cha kwanza mpaka Aprili, 2016 katika Wilaya ni kama unavyoonekana katika jedwali hapa chini,

Jedwali Na. 9: Udhili wa wanafunzi kidato cha kwanza

Wanafunzi	Jinsia		Jumla	Asilimia (%) dhidi ya lengo la 1409
	Wavulana	Wasichana		
Walioripoti	814	566	1380	98
Wasioripoti	8	21	29	2
Jumla	822	587	1409	

Chanzo: Idara ya Elimu sekondari Julai, 2016.

5.3 Hali ya taaluma kidato cha pili (FTSEE)

Hali ya ufaulu ya kidato cha Pili (FTSEE) matokeo yamekuwa mazuri yanaongezeka mwaka hadi mwaka. Mwaka 2013 ilikuwa asilimia 60, Mwaka 2014 yalikuwa asilimia 66 na Mwaka 2015 matokeo yamekuwa asilimia 87 sawa na ongezeko la asilimia 21.

5.4 Hali ya taaluma kidato cha nne (CSEE)

Hali ya ufaulu ya kidato cha Nne (CSEE) matokeo yamekuwa mazuri yanaongezeka mwaka hadi mwaka. Mwaka 2013 ilikuwa asilimia 57, Mwaka 2014 yalikuwa asilimia 64 na Mwaka 2015 matokeo yamekuwa asilimia 69.57

5.5 Hali ya taaluma kidato cha sita (ACSEE)

Hali ya ufaulu wa kidato cha Sita (ACSEE) matokeo yamekuwa mazuri yakiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka mwaka 2013 hadi 2015. Mwaka 2013 ilikuwa asilimia 94, Mwaka 2014 yalikuwa asilimia 100, Mwaka 2015 matokeo yalikuwa asilimia 100. Aidha kwa mwaka 2016, kati ya wanafunzi 153 waliofanya mtihani, waliofaulu ni 151 sawa na asilimia 98.7

5.6 Taarifa ya ujenzi wa maabara

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo ina shule 15 za Sekondari za Serikali ambapo shule moja tu ndiyo yenyewe maabara zote tatu zinazotumika ambayo ni shule ya sekondari Mambwe. Shule 14 zilizosalia ujenzi umefanyika kwa kuezeka majengo mawili ya Maabara. Kwa hatua hii iliyofikiwa, Halmashauri ilichangia Tsh. 19,001,050/= kwa kila Sekondari inayojenga Maabara. Aidha, Halmashauri katika bajeti yake ya mwaka 2015/16 ilitenga Tsh. 52,017,429/= kwa kila sekondari inayojenga maabara. Hadi sasa fedha hizi hazijapokelewa. Ujenzi wa maabara kwa sasa umesimama kutokana na kukosekana fedha.

5.7 Miundombinu ya shule kwa ujumla

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Hali ya miundombinu na samani katika shule za sekondari Wilayani Kalambo ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 10: Hali ya Miundombinu na samani katika idara ya Elimu Sekondari.

Miundombinu na Samani	Mahitaji	Iliyopo	% Uwepo	Upungufu	% Upungufu
Jengo la utawala	15	9	60.00	6	40.00
Vyumba vya madarasa	216	159	73.61	57	26.39
Maabara	45	3	6.67	42	93.33
Nyumba za walimu	318	78	24.53	240	75.47
Vyoo vya wanafunzi (Me)	183	123	67.21	60	32.79
Vyoo vya wanafunzi (Ke)	158	94	59.49	64	40.51
Vyoo vya walimu (Me)	26	17	65.38	9	34.62
Vyoo vya walimu (Ke)	24	17	70.83	7	29.17
Maktaba	15	0	-	15	100.00
Bwalo	15	0	-	15	100.00
Jiko	15	1	6.67	14	93.33
Viti vya Wanafunzi	4551	3420	75.15	1131	24.85
Meza za Wanafunzi	4551	3582	78.71	969	21.29
Meza za walimu	303	162	53.47	141	46.53
Viti vya walimu	316	212	67.09	104	32.91
Vitanda vya wanafunzi	1789	448	25.04	1341	74.96
Kasiki	21	14	66.67	7	33.33
Kabati	211	52	24.64	159	75.36

Chanzo: Idara ya Elimu sekondari Julai, 2016.

5.8 Taarifa ya mapokezi ya wanafunzi wa kidato cha tano.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo imepangiwa wanafunzi wa kidato cha tano 341, wote wakiwa ni wavulana. Mapokezi ya wanafunzi katika shule hizo ni kama inavyoonekana hapa chini katika jedwali,

Jedwali Na. 11: Mapokezi ya wanafunzi kidato cha tano

Shule	Waliopangwa	Walioripoti	% ya walioripoti	Hawajariipoti	% hawajariipoti
Mambwe	173	137	79.2	36	20.8
Matai	168	137	81.5	31	18.5
Jumla	341	274	80.4	67	19.6

Chanzo: *Idara ya Elimu sekondari, Julai 2016.*

Kwa mwaka 2016, kumekuwa na ongezeko la wanafunzi wa kidato cha tano kama ifuatavyo;

Shule ya Sekondari Mambwe ilikuwa na uwezo wa kupokea wanafunzi 70 lakini imeletewa wanafunzi 173 (ongezeko la 147.14%), halikadhalika Shule ya Sekondari Matai ilikuwa na uwezo wa kupokea wanafunzi 70 lakini imeletewa wanafunzi 169 (ongezeko la 141.4%), Jedwali lifuatalo linaonesha upungufu wa miundombinu unaotokana na ongezeko la wanafunzi wa kidato cha tano;

Jedwali Na. 12: Miundombinu katika shule za sekondari.

Miundombinu	Shule					
	Mambwe			Matai		
	hitaji	vilivyopo	Upungufu	hitaji	vilivyopo	Upungufu
madarasa	5	2	3	4	3	1
mabweni	3	1	2	3	2	1
vitanda	173	42	131	168	98	70
Matundu ya vyoo	16	16	0	12	7	5
Bafu	10	0	10	5	0	5

Chanzo: *Idara ya Elimu Sekondari, Julai 2016.*

Hata hivyo jitihada zimefanyika za kuhakikisha kwamba wanafunzi hawa wanaoripoti wanapata mahitaji yote ya msingi ikiwa ni pamoja na malazi kwa kuhakikisha vitanda vinatengenezwa kulingana na mapungufu yaliyojitokeza. Kwa upande wa mabweni, baadhi ya madarasa yanatumika kama mabweni wakati utaratibu wa kujenga mabweni ukiendelea.

6 TAARIFA YA MADAWATI.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo inaendelea na zoezi la utengenezaji wa madawati. Hapo awali Wilaya ilibainika kuwa na upungufu wa madawati yapatayo 12,198, ambapo kwa Shule za msingi zilikuwa na upungufu wa madawati 10,023 na shule za Sekondari madawati 2,175. Hadi kufikia Agosti, 2016 jumla ya madawati 9,371 yametengenezwa na mengine kukarabatiwa (sawa na asilimia 74.04 ya upungufu wa awali), na kufanya upungufu wa sasa kuwa madawati 2,827 (sawa na asilimia 22.2 ya upungufu wa awali). Jedwali hapa chini linaonesha hali halisi ya utengenezaji wa madawati kwa Shule za Msingi na Sekondari;

Jedwali Na. 13: Takwimu za madawati.

SHULE	MAHITAJI	YALIYOPO	UPUNGUFU	% UPUNGUFU
Shule ya Msingi	17,408	14,936	2,472	14.2
Shule Sekondari	4,351	3,996	355	8
JUMLA	21,759	18,922	2,827	22.2

Chanzo. Idara ya Elimu msingi na sekondari, Agosti 2016

6.1 Mikakati wa kukamilisha matengenezo ya madawati.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ina mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kuwa inakamilisha matengenezo ya madawati yaliyosalia kama inavyonekana hapa chini;

- i. Wilaya inaendelea na upasuaji wa mbao katika Hifadhi ya msitu wa Kalambo kwa eneo linalopisha ujenzi wa barabara.
- ii. Kuendelea kushirikisha wadau katika ngazi mbalimbali ndani na nje ya Wilaya ili kuchangia jitihada za Wilaya (Fund Raising) katika ukamilishaji wa utengenezaji wa madawati.
- iii. Kuongeza wigo wa makusanyo ya ndani ya Halmashauri kwa kutumia mashine za kielektroniki pamoja na kuziba mianya ya

upotevu wa mapato ili kuifanya Halmashauri kuwa na uwezo wa kutenga fedha za kutosha za Miradi pamoja na utengenezaji wa madawati.

6.2 Elimu bila malipo

Mheshimiwa waziri Mkuu,

Serikali katika kuboresha Uendeshaji wa Elimu ilianza kutoa fedha za Elimu bila malipo Desemba, 2015 kwa wanafunzi wote wanaosoma Elimu ya Awali, Msingi hadi Elimu ya Sekondari hadi kidato cha Nne. Fedha za Elimu bila malipo zimekuwa zikiingia kwenye akaunti za shule za msingi na sekondari kila mwezi. Ambapo kwa shule za msingi, fedha hizo zilizopokelewa na kutumika kuanzia mwezi Desemba hadi Julai ni shilingi 200,825,000/=.

Kwa upande wa Elimu ya Sekondari, Shule zote zimeendelea kupata fedha ya Elimu bila malipo kila mwezi ambapo tangu Mwezi Januari hadi Julai jumla ya shilingi 215,978,000/= zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Agizo la Serikali la kutekeleza Elimu msingi Bila Malipo limekuwa na mafanikio makubwa kwani:- asilimia ya uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza imeongezeka kutoka 94.7% ya Mwaka 2015 hadi 150.1% ya sasa. Pia mahudhurio ya wanafunzi kwa shule za msingi kutoka 86.3% (2015) hadi 97.2% (2016) na kwa shule za sekondari yameongezeka kutoka 86% (2015) hadi 95% (2016)

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Tunaipongeza na kuishukuru serikali kwa mikakati yake mizuri ya kuboresha Elimu nchini ikiwa ni pamoja na kufanya yafuatayo; -

- i. Kutoa fedha za Elimu msingi bila malipo kila mwezi kila kila shule nchi nzima.
- ii. Kutoa vitabu vya darasa la kwanza na la pili nchi nzima
- iii. Kuendesha mafunzo ya elimu ya awali na msingi kwa walimu
- iv. Kutoa madawati (kiti na meza) 861 kutoka serikali kuu na madawati 537 kutoka Mfuko wa Jimbo

- v. Kuendesha mafunzo kwa walimu wa masomo ya sayansi, Hisabati na masomo ya lugha kwa shule za Sekondari na,
- vi. Kuwajengea uwezo walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Waratibu Elimu Kata.

7 TAARIFA YA UTOAJI HUDUMA ZA AFYA

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo ina jumla ya vituo vya kutolea huduma za Afya 59, kati ya hivyo, vituo vya afya 4 na zahanati 55. Zahanati 5 kati ya 55 zinaendeshwa na mashirika ya dini (FBOs).

7.1 Hali ya watumishi na utumishi katika sekta ya afya

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo katika Sekta ya Afya ina jumla ya watumishi 373 (sawa na asilimia 44) kati ya 847 wanaohitajika, hivyo kufanya upungufu kuwa wafanyakazi 474 (sawa na asilimia 56).

Jedwali Na. 14: Hali halisi ya Watumishi katika Sekta ya Afya

NA	KADA	MAHIT AJI	WALIO PO	%	UPUNGUFU	%
1	MD	4	1	25	3	75
2	AMO	16	4	25	12	75
3	CO/CA	65	47	72	18	28
4	NO	2	1	50	1	50
5	ANO	16	9	56	7	44
6	EN	186	97	52	89	48
7	MATT	89	171	192	-82	-92
8	EHO	6	0	0	6	100
9	AEHO	23	6	26	17	74
10	H/Asst	111	3	3	108	97
11	LAB/ASS	59	24	41	35	59
12	HLAB TECH	8	0	0	8	100
13	Dental therapist	4	0	0	4	100
14	Assistant Dental officer	4	0	0	4	100
15	Pharmaceutical technologist	4	0	0	4	100

NA	KADA	MAHIT AJI	WALIO PO	%	UPUNGUFU	%
16	Pharmaceutical Ass. techn	59	2	3	57	97
17	Nutritional officer	3	2	67	1	33
18	Community health worker	59	0	0	59	100
19	Social Welfare officer	1	1	100	0	0
20	Ass. Social Welfare officer	4	0	0	4	100
21	Health secretary	2	3	150	-1	-50
22	Security	122	2	2	120	98
JUMLA		847	373	44	474	56

Chanzo: Ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya, Julai 2016.

7.2 Miundombinu, samani na vifaa vya usafiri katika idara ya afya.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo kwa upande wa hali ya miundombinu, samani na vifaa vya usafiri katika Sekta ya Afya ni kama ifuatavyo:-

Jedwali Na. 15: Hali ya Miundombinu,samani na vifaa vya usafiri.

Miundombinu na Samani	Mahitaji	Iliyopo	% Uwepo	Upungufu	% Upungufu
Hospitali ya wilaya	1	0	0	1	100
Vituo vya afya	23	4	17	19	83
Zahanati	111	55	50	56	50
Maduka ya dawa	120	80	67	40	33
Maabara	59	10	17	49	83
Vitanda vya wagonjwa	380	132	35	248	65
Viti vya wagonjwa (Wheel chair)	28	7	25	21	75
Nyumba za watoa huduma	185	31	17	154	83
Magari (Ambulance)	5	0	0	5	100
Magari ya kawaida	6	2	33	4	67
Pikipiki (Miguu mitatu)	10	2	20	8	80

Miundombinu na Samani	Mahitaji	Iliyopo	% Uwepo	Upungufu	% Upungufu
Pikipiki (Miguu miwili)	59	14	24	45	76
Boti (Ambulance)	2	1	50	1	50
Boti ya kawaida	1	1	100	0	0

Chanzo: Ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya, Julai, 2016.

7.3 Magonjwa kumi (10) yanayoathiri zaidi wananchi Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Katika Wilaya ya Kalambo magonjwa kumi (10) yanayoathiri zaidi wananchi ni malaria, magonjwa yanayoathiri mfumo wa upumuaji, kuhara, vichomi, magonjwa ya yanayoathiri mfumo wa mkojo (U.T.I), minyoo ya tumbo, pumu, magonjwa ya ngozi, magonjwa ya macho na magonjwa yanayohitaji upasuaji mdogo kama majipu.

Aidha wagonjwa wa nje kwa mwaka wa fedha 2015/2016 wamepungua kwa asilimia 14.5 ukilinganisha na mwaka 2014/2015 pia wagonjwa wa ndani wamepungua kwa asilimia 30.4

Jedwali Na. 16: Idadi wagojwa wa nje na ndani

Wagonjwa	Mwaka		Tofauti	% Tofauti
	2014/2015	2015/2016		
Wagonjwa wa nje	108,788	95,014	13,774	14.5
Wagonjwa wa ndani	1,411	1,082	329	30.4

Chanzo: Ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya, Julai, 2016.

7.4 Huduma za chanjo ya mama na mtoto Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo inaendelea na zoezi la utoaji chanjo ya mama na mtoto na kutoa elimu kwa Jamii juu ya chanjo hizo kuitia Sekta ya Afya. Kwa kipindi cha Januari mpaka Disemba, 2015 wastani wa watoto 11,000 walipatiwa chanjo (sawa na Asilimia 99.4) kati ya watoto 11,069, pia kati ya akina mama 11,069 waliopatiwa chanjo ya pepopunda (T.T 2+) ni 8,264 (sawa na asilimia 74.6).

Halikadhalika kwa kipindi cha Januari mpaka Mei, 2016 wastani wa watoto 5,349 walipatiwa chanjo (sawa na Asilimia 52.0) kati ya watoto 10,348, pia kati ya akina mama 10,348 waliopatiwa chanjo (T.T 2+) ni 2,680 (sawa na asilimia 25.9).

Jedwali Na. 17: Chanjo zitolewazo na idadi ya walengwa

Na.	Aina ya chanjo	Januari hadi Disemba, 2015			Januari hadi May, 2016		
		Idadi ya Walengwa	Idadi ya Waliopati wa chanjo	%	Idadi ya Walengwa	Idadi ya Waliopati wa chanjo	%
1	BCG	11,069	11,046	99.8	10,348	7,330	70.8
2	DPT – HB	11,069	11,046	99.8	10,348	4,836	46.7
3	OPV – 3	11,069	10,952	98.9	10,348	5,008	48.4
4	ROTA-2	11,069	10,886	98.3	10,348	4,935	47.7
5	MEASLES /Rubella	11,069	11,029	99.6	10,348	5,104	49.3
6	PCV -3	11,069	11,043	99.8	10,348	4,879	47.1
7	T.T -2+	11,069	8,262	74.6	10,348	2,680	25.9

Chanzo: Ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya, Julai 2016

7.5 Mafanikio katika utoaji wa huduma za afya.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo kuitia Sekta ya Afya Katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2016 katika jitihada za kuboresha utoaji na upatikanaji wa huduma za Afya imefanikiwa katika maeneo yafuatayo:-

- i. Halmashauri kwa kushirikiana na wadau imefanikiwa kujenga vyumba vitatu vya upasuaji katika vituo vya Afya Matai, Mwimbi na Ngorotwa.
- ii. Tumefanikiwa kupunguza utapiamlo uliokithiri (ukondefu) kutoka asilimia 4 kwa mwaka 2014/2015 hadi kufikia asilimia 2 kwa 2015/2016. Aidha tumefanikiwa kupunguza watoto wenye

- uzito pungufu kutoka asilimia 3 kwa mwaka 2014/2015 hadi asilimia 2 kwa mwaka 2015/2016.
- iii. Tumefanikiwa kuwapatia wazee 1,250 wenyewe umri wa miaka zaidi ya 60 vitambulisho ili waweze kupata huduma za afya bure kama sera ya Serikali inavyosema, sawa na asilimia 21 ya wazee 5,885 waliotambuliwa.
 - iv. Madirisha maalumu yameanzishwa katika vituo vya afya kwa ajili ya wateja wa CHF na NHIF pamoja na wazee kwa vituo 3 vya afya ili kuhamasisha uchangiaji wa mfuko wa Bima ya afya ya jamii (CHF). Hata hivyo juhudini za kufungua madirisha ya wazee katika vituo vilivyobakia, zinaendelea ili kukamilisha zeozi hilo.
 - v. Tumefanikiwa kuongeza idadi ya akina mama wajawazito wanaojifungulia katika vituo vya afya na zahanati kutoka asilimia 62 ya mwaka 2013/14 hadi kufikia asilimia 93 mwaka 2015/16.
 - vi. Tumeongeza idadi ya wateja wapya wa uzazi wa mpango kutoka asilimia 46 mwaka 2014/15 hadi asilimia 48.5 mwaka 2015/16.
 - vii. Tumefanikiwa kupunguza maambuzi ya virusi vya ukimwi kutoka asilimia 2.6 mwaka 2014/15 hadi asilimia 1.5 mwaka 2015/16.
 - viii. Kiwango cha malaria kimepungua kwa asilimia 4.8% kutoka asilimia 30 mwaka 2014/15 hadi kufikia asilimia 25.2 mwaka 2015/16.
 - ix. Tumeimarisha ufuatiliaji wa magonjwa ya milipuko na yale yanayozuilikia kwa chanjo pamoja na kuimarisha uratibu wa ufuatiliaji wa magonjwa mipakani kati ya Tanzania na Zambia.
 - x. Usimamizi elekezi ulifanyika katika vituo vyote 59 kwa kila robo mwaka.
 - xi. Kununua na kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo 59.

- xii. Huduma za upasuaji zilitolewa kwa mama wajawazito 151, ambapo kituo cha afya Mwimbi akina mama 21 na kituo cha afya Matai akina mama 130 wamefanyiwa upasuaji.
- xiii. Tumepandisha idadi ya wanachama wa CHF kutoka asilimia 5 mwaka 2014/15 hadi asilimia 15 mwaka 2015/16.
- xiv. Tumeboresha huduma za maabara katika kituo cha afya Matai kwa kufunga vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa magonjwa mbalimbali.
- xv. Tumeanzisha huduma za uchunguzi wa kansa ya shingo ya kizazi kwa wanawake katika kituo cha afya Matai.

8 USAFI WA MAZINGIRA

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo imeendelea kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais kwa kufanya usafi wa mazingira kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi na Jumamosi ya kila wiki, ambapo wananchi na watumishi hushiriki katika maeneo yao. Usafi wa mazingira pia umekuwa ukifanyika katika maeneo ya kufanya biashara kama vile, masoko, maduka, migahawa, nyumba za kulala wageni, barabara na mifereji ya maji ya mvua.

9 SEKTA YA MAJI

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo katika sekta ya maji ina jumla Watumishi 6 kati ya Watumishi 28 wanaotakiwa kwa mujibu wa ikama. Kati ya watumishi hao Mhandisi ni mmoja (1), Fundi Sanifu wanne (4), na Fundi Sanifu Msaidizi mmoja (1).

9.1 Upatikanaji wa huduma ya maji

Wilaya ina visima vifupi 14 vinavyofanyakazi na 25 visivyofanyakazi, visima virefu 68 vinavyofanyakazi na 63 visivyofanya kazi, miradi ya bomba ya mtiririko 8 inayofanya kazi na 4 isiyofanyakazi, miradi miwili ya maji ya kusukuma kwa mashine chemichemi zilizohifadhiwa 10 na miundombinu ya kuvuna maji ya mvua katika taasisi

mbalimbali. Aidha miradi yote tajwa hapo juu ina jumla ya vituo 463 ambapo vituo 316 vinafanyakazi vinakadiria kuhudumia wananchi wapatao 96,200.

Wilaya ya Kalambo inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa mpango wa vijiji 10 na vijiji vya nyongeza yaani vya ***Quickwins***.

Miradi iliyotekelwa kuitia Miradi ya maendeleo ya maji ni.

- a. Mradi wa maji wa Mserereko wa Matai. Mradi huu umekamilika japo vituo vinne havitoi maji.
- b. Mradi wa maji ya kisima wa kijiji cha Mwimbi; mradi huu upo hatua za ukamilishaji, marekebisho katika tenki la maji yanafanyaika
- c. Mradi wa maji ya mserereko wa kijiji cha Kisumba; mradi huu umekamilika na unatoa huduma.
- d. Mradi wa maji Kasanga; Mradi huu umekamilika na unatoa huduma. Changamoto ni maji kutofika kwa baadhi ya siku katika vituo 2 katika kitongoji cha songambele
- e. Mradi wa maji wa Kamawe; mradi huu umekamilika na wananchi wanapata huduma ya maji
- f. Mradi wa maji wa Mwazye. Mradi huu umekamilika kwa ujenzi wa tenki, Miundombinu ya kutawanya maji na vituo vya kuchotea maji. Mradi huu upo katika hatua ya kubadilisha usanifu kutoka katika ukarabati wa chanzo kilichopo kwenda chanzo kipyka kutokana na chanzo hicho kuchafuliwa na mifugo pamoja na binadamu kutengeneza njia ya kwenda katika vijiji vya pembezoni

10 SEKTA YA UJENZI

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo katika Sekta ya Ujenzi ina jumla ya watumishi kumi na wawili (12) ambao kati ya hao, Wahandisi ni watano (5), Fundi sanifu watano (5) pamoja na Madereva wawili (2). Wilaya inahudumia

mtando wa barabara wenyе urefu wa Km. 846.6 ambapo kati ya hizo Km. 188.1 ni za kiwango cha changarawe na Km. 652.5 ni za udongo. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wilaya imeidhinishiwa kiasi cha Tshs. 643,530,000.00

10.1 Utekelezaji wa miradi ya ujenzi

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Mpaka sasa Wilaya katika Sekta ya Ujenzi inaendelea kutekeleza miradi ya mwaka wa Fedha 2014/2015 ambapo miradi tisa (9) imekamilika na miradi mitatu (3) inaendelea.

Jedwali Na. 18: Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi

Na.	JINA LA MRADI	UREFU (Km.)	HALI YA MRADI
1	Kiundi – Madibila	10.2	Umekamilika
2	Myunga – Kaengesa Mikonko – Sengakalonje	7.5 18	Umekamilika
3	Mtula – Mosi	8.5	Umekamilika
4	Mkombo – Mlenje	13	Umekamilika
5	Msanzi – Mao	10	Umekamilika
6	Chelenganya – Katuka	5	Umekamilika
7	Kasanga – Kilewani	3	Umekamilika
8	Kalembe – Utengule	12	Umekamilika
9	Kawala – Kapozwa	16	Umekamilika
10	Kifone – Ilambila	7	Haujakamilika
11	Katazi – Kafukula – Kanyezi	20	Haujakamilika
12	Kaluko – Ngoma – Kamawe	11.5	Haujakamilika

Chanzo: *Idara ya Ujenzi, Julai, 2016*

10.2 Miradi ya mwaka wa fedha 2015/2016

Miradi mitatu ya barabara kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kazi zimeanza kutekelezwa Julai 2016 na miradi mingine mitatu ya barabara kwa mwaka 2015/16 ipo katika hatua ya manunuizi.

10.3 Mapokezi ya fedha

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016 Wilaya imepokea kiasi cha Tsh 927,864,464.84 ambapo kati ya hizo shilingi 888,765,390.80 ni kwa

ajili ya miradi ya mwaka wa Fedha 2014/2015 na shilingi 39,099,074.04 ni mapokezi ya fedha za miradi ya mwaka wa Fedha 2015/2016.

11 TAARIFA YA UJENZI WA NYUMBA ZA VIONGOZI WAANDAMIZI WA WILAYA

11.1 Taarifa ya mradi wa nyumba za viongozi katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kalambo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Mradi huu ni moja ya Miradi inayotekelawa na Kikosi cha ujenzi cha Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) katika Mkoa wa Rukwa. Mshitiri wa mradi huu ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Mradi huu unajengwa kwa utaratibu wa 'Usanifu na Kujenga' (Design and Build). Nyumba zinazojengwa ni nyumba ya makazi ya Mkuu wa Wilaya, Nyumba ya makazi ya Katibu Tawala Wilaya na nyumba mbili za makazi ya viongozi waandamizi wa Wilaya. Thamani ya mradi huu ni Tsh. 506,706,144.00. Mradi ulikuwa wa muda wa wiki 32 kuanzia tarehe 14/8/2014 na ultakuwa kukamilika tarehe 6/5/2015.

Kwa sasa mradi huu umesimamishwa na Katibu Mkuu, OR – TAMISEMI. Hadi wakati mradi unasitishwa, ujenzi ulikuwa unaendelea kwa nyumba ya Mkuu wa Wilaya, Katibu Tawala wa Wilaya na nyumba mbili za Maafisa Waandamizi. Kutokana na ukosefu wa nyumba hizo, viongozi wanaishi katika nyumba za kupanga.

11.2 Taarifa ya ujenzi wa nyumba saba za watumishi wa Halmashauri

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Mradi wa Ujenzi wa nyumba saba (7) za watumishi ulisainiwa tarehe 30.04.2015 kati ya Mkurugenzi Mtendaji (W) wa S. L. P. 03, Matai – Kalambo na Mkandarasi M/s. Kosemwa Prospects Co. Ltd wa S. L. P. 42135, Dar es Salaam kwa gharama ya shilingi 496,037,500.00 na

muda wa utekelezaji wa miezi minne (4) ambapo kazi ilianza tarehe 04.05.2015 na kutakiwa kukamilika tarehe 07.09.2015

Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mradi:

Baada ya kusainiwa kwa Mkataba, mradi wa nyumba saba (7) ulianza kutekelezwa vizuri na kwa kasi ya kuridhisha ambapo Mkandarasi alichimba misingi yote saba (7) na ujenzi wa misingi ya nyumba tano (5) kwa kutumia mawe na kisha kumwaga jamvi.

Baada ya Kukamilika kwa ujenzi wa misingi ya nyumba Mkandarasi alianza kujenga kuta za nyumba tano kwa kutumia tofali za kuchoma. Hata hivyo Mkandarasi akiwa anaendelea na kazi za ujenzi ilionekana vyumba kutokukidhi haja ya watumiaji na baadhi ya kuta kutokuwa na ubora, hivyo Mkandarasi aliamriwa kuvunja kuta hizo.

Ili kuboresha kazi ilionekana ni vema kubadili ramani ya nyumba pamoja na kutumia tofali za “blocks” ambapo hadi sasa mkandarasi anaendelea na kazi ya ujenzi wa kuta kwa kutumia tofali za “blocks”.

Baada ya mabadiliko hayo yote kufanyika, muda wa kukamilisha kazi hizo zote ulibadilika na kuwa tarehe 01.01.2017

Malipo:

Mpaka sasa Mkandarasi amelipwa shilingi 121,739,200.00 ikiwa ni kwa kazi alizozifanya mpaka hatua msingi.

12 SEKTA YA KILIMO

Mheshimiwa Waziri Mkuu

Wilaya ya Kalambo ina ukubwa wa hekta 471,500 kati ya hizo, hekta 319,300 zinafaa kwa kilimo sawa na asilimia 76.47. Eneo linalolimwa kwa sasa ni hekta 129,921.76 sawa na asilimia 41 ya eneo lote linalofaa kwa kilimo.

12.1 Hali ya chakula msimu wa mwaka 2015/16.

Mheshimiwa Waziri Mkuu

Wilaya kuitia Idara ya kilimo, Umwagiliaji na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ilipanga kuzalisha mazao mbalimbali kwa kulima hekta 129,921.76 kwa matarajio ya kuvuna tani 340,542.45. Mpaka sasa kwa zao la mahindi linalotegemewa kwa chakula hali halisi ya mavuno ni tani 104,020.6. Uhitaji wa chakula kwa Wilaya nzima ni tani 69,000 za mahindi na kufanya ziada ya tani 35,020.6 za mahindi

12.2 Mfumo wa utoaji wa pembejeo za ruzuku 2015/2016.

Mheshimiwa Waziri Mkuu

Serikali imeendelea kutoa ruzuku za pembejeo za kilimo ili kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao ya chakula ambayo ni mahindi kwa njia ya utaratibu wa Vocha. Wilaya imepata mgawo wa jumla ya Vocha zipatazo 51,294 ikiwa vocha 17,098 mbegu chotara, vocha 17,098 mbolea ya kukuzia na vocha 17,098 mbolea ya kupandia. Vocha zipatazo 51,294 ziligawanywa na kusambazwa katika Kata 23 na vijiji 111. Jumla ya Vocha 15,371 kati ya vocha 17,098 za mboela ya kupandia zimetumika sawa na asilimia 89.89%. Vocha za mbolea ya kukuzia zilizotumika ni vocha 15,566 kati ya vocha 17,098 sawa na asilimia 91.03% na vocha za mbegu chotara ya Mahindi zilizotumika ni 13,735 kati ya 17,098 sawa na asilimia 73.31%.

Jedwali Na. 19: Mgawanyo wa vocha za pembejeo zilizogawiwa kwenye ngazi ya kata na idadi ya vocha zilizotumika.

KATA	KIASI CHA VOCHA KILICHOGAWIWA			KIASI CHA VOCHA ZILIZOTUMIKA			IDADI YA VOCHA ZILIZORUDISHWA		
	DAP	UREA	MBEGU	DAP	UREA	MBEGU	DAP	UREA	MBEGU
Msanzi	865	865	865	793	800	200	72	65	665
Matai	750	750	750	698	716	595	52	34	155
Mkali	750	750	750	750	750	750	0	0	0
Mkowe	700	700	700	700	700	471	0	0	229
Sopa	800	800	800	800	800	800	0	0	0
Katete	1000	1000	1000	1000	1000	1000	0	0	0
Mwazye	900	900	900	600	600	0	300	300	900
Kilesha	1000	1000	1000	1000	1000	1000	0	0	0
Katazi	1000	1000	1000	800	800	800	200	200	200
Kanyezi	400	400	400	400	400	200	0	0	200
Mwimbi	1300	1300	1300	1200	1300	1200	100	0	100
Ulumi	1200	1200	1200	1200	1200	1200	0	0	0
Mnamba	998	998	998	849	866	791	149	132	207
Mambwekenya	1000	1000	1000	944	960	425	56	40	575
Mambwekoswe	1300	1300	1300	1241	1212	1201	59	88	99
Legezamwendo	1000	1000	1000	430	438	609	570	562	391
Lyowa	800	800	800	672	718	543	128	82	257

KATA	KIASI CHA VOCHA KILICHOGAWIWA			KIASI CHA VOCHA ZILIZOTUMIKA			IDADI YA VOCHA ZILIZORUDISHWA		
	DAP	UREA	MBEGU	DAP	UREA	MBEGU	DAP	UREA	MBEGU
Mbuluma	600	600	600	600	600	600	0	0	0
Sundu	500	500	500	500	500	2	0	0	498
Kisumba	50	50	50	40	50	20	10	0	30
Mpombwe	65	65	65	45	45	40	20	20	25
Samazi	60	60	60	58	59	47	2	1	13
Kasanga	60	60	60	51	52	41	9	8	19
Jumla	17098	17098	17098	15371	15566	12535	1727	1532	4563

Chanzo: Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika Julai 2016

12.3 Changamoto za mfumo wa utoaji pembejeo

1. Makampuni ya pembejeo kushindwa kuwakopesha mawakala pembejeo hivyo kushindwa kusambaza pembejeo kwa wakati.
2. Kupanda kwa gharama za uchangiaji kwa wanufaika tofauti na waraka wa pembejeo wa mwaka 2015/16.
3. Kuchelewa kwa usambazaji wa vocha za pembejeo kwani Wilaya ya Kalambo mvua huanza kunyesha mapema mwezi wa kumi hivyo maandalizi yanaanza mwezi Septemba.

12.4 Mipango inayolenga kuleta matokeo makubwa (BRN)

Wilaya ya Kalambo kuitia sekta ya kilimo ni moja kati ya wilaya zinazotekeleza Miradi ya BRN kwa kukarabati maghala ya kuhifadhi mahindi. Katika kipindi cha Mwaka wa fedha 2014/2015 Wilaya ilipangiwa kukarabati maghala 9 ya vijiji vya Msanzi, Matai, Mwazye, Mambwekenya, Ulumi, Majengo, Ilambilila na Kizombwe yenyewe uwezo wa kuhifadhi tani 3,600. Ambapo mpaka sasa maghala saba (7) yamekamilika na mawili (2) yapo katika hatua ya mwisho ya ukamilishaji.

Jedwali Na. 20: Ukarabati wa wa Maghala tisa (9)

KATA	KIJIJI	CAPACITY (UWEZO)/TANI	HALI YA UKARABATI ILIGO FIKIA
MSANZI	MSANZI	500	Umekamilika
MATAI	MATAI	400	Umekamilika
MWAZYE	MWAZYE	300	Hatua ya kazi za nyongeza
M/KENYA	M/KENYA	500	Umekamilika
ULUMI	ULUMI	300	Umekamilika
MWIMBI	MAJENGKO	500	Hatua za mwisho
ULUMI	KALEPULA	300	Umekamilika
SOPA	ILAMBILA	300	Umekamilika
MKALI	KIZOMBWE	500	Umekamilika
JUMLA		3600	

Chanzo: Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika, Julai 2016

12.5 Maandalizi ya ununuzi wa mahindi kupitia NFRA.

Mheshimiwa Waziri Mkuu

Wilaya ya Kalambo kwa kushirikiana na wakala wa Taifa wa hifadhi ya chakula NRFA imekamilisha maandalizi na ukaguzi wa vituo vitakavyo husika kununulia mahindi kwa msimu huu, hadi sasa ununuzi wa mahindi ni kama unavyoonekana katika jedwali hapo chini.

Jedwali Na. 21: Maandalizi ya ununuzi wa mahindi kupitia NFRA

S/N	JINA LA KITUO CHA UNUNUZI	IDADI YA TANI WALIZOPANGIWA	IDADI YA TANI ZILIZO NUNULIWA HADI KUFIKIA 19/08/2016
1	Soko la Matai	750	Tani 338.58
2	Sopa (KANYELE AMCOS)	150	Tani 120
3	Mkali (AMCOS)	150	Tani 50
4	Mwimbi	500	Tani 375
5	Katazi	325	Tani 325
6	Msanzi(MUZIA AMCOS)	700	Tani 210
7	MKUSA AMCOS	150	Tani 90
JUMLA KUU		3225	1508.58

Chanzo: Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika Agosti, 2016

12.6 Kuanzisha uzalishaji wa zao wa kahawa

Mheshimiwa Waziri Mkuu

Wilaya ya Kalambo imeanzisha uzalishaj zao la kahawa ili kuwa na zao la biashara lenye tija na kuongeza uchumi wa Wilaya na wakulima kwa ujumla. Ili kutekeleza mradi huu, Wilaya imeotesha mbegu kwenye viriba katika Msitu wa Serikali wa Mbizi Forest Reserve ambapo hadi sasa imefikia hatua ya kupandikiza. Baadhi ya Vijiji vilivyofanikiwa kupata miche hiyo ni Msanzi, Katuka, Singiwe, Mbuba na Ilimba. Jumla ya miche 15,000 imeshapandwa na wakulima wa vijiji vya Msanzi, Katuka na Singiwe.

12.7 Kuanzisha uzalishaji wa zao la ufuta

Mheshimiwa Waziri Mkuu

Wilaya pia imeanzisha uzalishaji wa zao la ufuta kama zao mbadala la biashara lenye tija na kuongeza uchumi wa Wilaya. Vijiji ambavyo mbegu zimepelekwa kwa majaribio ya uzalishaji wa zao hili ni Kalembe, Chipapa, Kantalemwa na Luse. Maeneo ya kata za Kisumba, Mpombwe na Samazi ufuta unastawi vizuri sana hivyo hamasa ya kuwahamasisha wakulima kulima zao la ufuta kwa biashara inaendelea.

12.8 Kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Waziri Mkuu

Wilaya ya Kalambo ina jumla ya hekta 4,500 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, kati ya eneo hilo hekta 650 sawa 14.4% ya eneo lote ndio linatumika kwa shughuli za kilimo cha umwagiliaji kwa sasa kupitia miundombinu ya kisasa iliyopo. Skimu za umwagiliaji zinazotumika kwa kilimo ndani ya Wilaya ya Kalambo ni pamoja na skimu ya umwagiliaji ya Katuka, Skimu ya umwagiliaji ya Singiwe na skimu ya umwagiliaji ya Ulumi kama zilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 22: Hali ya skimu za Umwagiliaji

Halmashauri	Jina la skimu	Eneo	Eneo linalotumika kwa sasa	Aina ya umwagiliaji, Asili/kisasa
Kalambo	Singiwe	1000	250	Kisasa
	Ulumi	1000	-	
	Katuka	2500	400	Kisasa
JUMLA		4500	650	

Chanzo: Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika Julai 2016

12.9 Hali ya vyama vya ushirika

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Vyama vya ushirika vimeendelea kukua kufikia vyama vya ushirika 22, ambapo vyama 15 ni vya kuweka na kukopa (SACCOS), Vyama vya ushirika vya mazao (AMCOS) vimefikia vitano (5), Chama cha ushirika cha wafugaji kimoja (1) na Chama cha ushirika cha wavuvi kimoja (1) na kufanya jumla ya vyama vya ushirika Wilaya ya Kalambo kufikia vyama 22.

Kwa sasa vyama vya ushirika vimefanikiwa kuongeza idadi ya wanachama, kuongeza idadi ya hisa, Akiba za wanachama na Amana za wanachama. Vyama vya ushirika Wilaya ya Kalambo vina jumla ya wanachama 2,702. Wanachama hao wapo kwenye makundi yafuatayo, wanawake ni 1,621, wanaume 1,053 na vijana 28. Vyama vya ushirika Wilaya ya Kalambo vina Hisa zenye thamani ya shilingi 38,140,800, Akiba za shilingi 139,934,284 na Amana za shilingi 400,500.

Vyama vya ushirika Wilaya ya Kalambo vimepokea mikopo yenye thamani ya shilingi 804,595,000 kutoka taasisi mbalimbali za fedha na wadau wengine wa maendeleo. Kati ya fedha hizo vyama vya ushirika vimefanikiwa kurejesha shilingi 531,683,111 na kubaki shilingi 272,988,991/= ambazo bado vyama vinaendelea kurejesha ili kuweza kukopa upya.

13 SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya katika idara ya Mifugo na Uvubi ina jumla ya watumishi 21, kati ya hao watumishi 6 wako makao makuu ya Wilaya na watumishi 15 wapo ngazi ya kata na vijiji, huku ikiwa na upungufu wa watumishi 140 katika sekta ya Mifugo na Uvubi.

13.1 Idadi ya mifugo na wafugaji.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo ina jumla ya Ng`ombe 91,325, Mbuzi 28,063, Kondoo 3,386, Punda 1,756, Nguruwe 5,078, Kuku 67,461, Bata 1,958, Kanga 565, Njiwa 2,957, Paka 2,095 na Sungura 1,350

13.2 Huduma za mifugo

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya imeendelea kutoa elimu kwa wafugaji juu ya ufugaji bora na wenye tija, Utoaji wa chanjo na tiba kwa mifugo dhidi ya magonjwa mbalimbali kupitia wataalam waliopo makao makuu ya Wilaya na wale wa ngazi ya Kata na Vijiji. Chanjo zilizotolewa ni pamoja na Chanjo dhidi ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa (Rabies), Kamkono (BQ), Homa ya Mapafu (CBPP) na Kideri (NCD).

13.3 Soko la mifugo

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Kwa sasa Wilaya ya Kalambo ina jumla ya masoko matatu ya mifugo ambayo ni Kasesya (Katete), Mtula (Mnamba) na Mkowe. Hali ya soko la mifugo katika Wilaya ya Kalambo ni ya kuridhisha.

13.4 Hali ya miundombinu

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo kwa sasa in jumla ya majosho 15 kati ya haya majosho 7 ni ya watu binafsi na majosho 8 ni ya serikali. Uwepo wa majosho haya umepunguza kwa kiasi kikubwa magonjwa yatokanayo na kupe. Aidha Wilaya ina vituo vya kuendeleza mifugo viatau (3) (*Livestock Development centres*) vilivyopo katika vijiji cha Mwazye, Kale na Msanzi. Wilaya ina machinjo - makaro 3 (*Slaughter slabs*) katika vijiji vya Katete (Kasesya), Mwazye na katika mji wa Matai.

Jedwali Na. 23: Hali ya miundombinu katika sekta ya Mifugo na Uvuvi

Na.	AINA YA MIUNDOMBINU	HITAJIKA	ILIYOPO	UPUNGUFU
1	Josho	23	15	8
2	Jengo la Mnada	3	1	2
3	Machinjio	23	3	20
4	Nyumba za Watumishi	23	2	21
5	Vituo vya kuendeleza mifugo (<i>Livestock Development Centre</i>)	5	3	2
JUMLA		77	24	53

Chanzo: Idara ya Mifugo na Uvuvi Julai 2016

13.5 Migogoro baina ya wafugaji na wakulima

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Kuna migogoro baina ya wafugaji na wakulima iliyojitokeza katika baadhi ya maeneo hususan katika kata za Legezamwendo, Kanyezi na Mambwenkoswe. Wilaya imeshafanya mikutano mbalimbali kati ya wafugaji na wakulima ikiwa ni pamoja na kutoa miongozo kuhusu uhamishaji wa mifugo kutoka sehemu moja hadi nyingine.

14 SEKTA YA UVUVI

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo ina jumla ya wavuvi 2,615 wanaojishughulisha na shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika na mabwawa yanayofaa kwa shughuli za uvuvi na ufugaji wa samaki hususani katika kata za Kasanga, Samazi, Kisumba, Sundu, Kilesha na Mpombwe.

14.1 Vyombo vya uvuvi

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Kwa mujibu wa sensa ya uvuvi ya mwaka 2011 kupitia mradi wa ziwa Tanganyika, Wilaya ya Kalambo inakadirisha kuwa na Mitumbwi 1,023, Mashine za boti 213, nyavi za kipe 32, Nyavi za kuzungusha (*Ring Net*) 145 na Ndoana 22,499.

14.2 Miundombinu ya uvuvi

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo ina miundombinu mbalimbali ya uvuvi katika mwambao wa ziwa Tanganyika ambayo ni:-

- i. Mialo 18 ya uvuvi ambayo yote ni ya asili
- ii. Soko la samaki la Kasanga, soko hili limejengwa kwa ubia baina ya Serikali na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA). Mradi wa MIVARF unaedelea na taratibu za ukamilishaji wa miundombinu itakayowezesha soko hili lianzu kutumika.

15 SEKTA YA ARDHI.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya kuitia Sekta ya Ardhi imeendelea na majukumu yake ya upimaji wa viwanja, upangaji miji, utatuzi wa migogoro ya Ardhi na umilikishaji wa Ardhi kwa mujibu wa kanuni, taratibu na sheria.

15.1 Upimaji wa viwanja na vijiji.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Hadi kufikia Agosti 2016, maeneo mbalimbali ya Wilaya yamepimwa ambapo jumla ya viwanja 1,538 vimepimwa kama inavyoonyesha kwenye jedwali hapo chini.

Jedwali Na. 24: Maeneo yaliyopimwa viwanja.

Eneo/Kata	Lyowa	Kasanga	Matai	Mikonko	Kapozwa	Mkangale
Idadi ya viwanja	182	414	531	34	365	12

Chanzo: Idara ya Ardhi Agosti 2016

15.2 Utoaji wa hati miliki.

Jumla ya hati miliki 331 za kisheria na hati miliki za kimila 390 zimetolewa.

15.3 Mpango wa uandaaji wa ‘Master Plan’ ya miji yetu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Kutokana na gharama kubwa za uandaaji wa master plan, mpaka sasa Wilaya haijaweza kuandaa ‘Master Plan’. Katika kukabiliana na changamoto hiyo Wilaya kuitia idara ya Ardhi imeandaa michoro ya mipango miji 16 yenye viwanja 6,170 vya matumizi mbalimbali na upimaji zaidi unaendelea ili kuzuia ujenzi holela.

15.4 Ulipaji wa fidia kwenye maeneo yaliyofanyiwa uthamini.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya kuitia idara ya ardhi imefanya uthamini kwa ajili ya fidia kwa wananchi 47 ambao maeneo yao yalitwaliwa kupisha uchimbaji wa mfereji wa kuzuia maji toka mlimani, ujenzi wa barabara na baadhi ya maeneo yaliyopimwa viwanja. Hadi kufikia tarehe 30, Julai 2016 wananchi 7 kati ya 47 wamelipwa kiasi cha shilingi 4,960,632 fedha zilizotokana na mauzo ya fomu za maombi ya viwanja. Pia tutaendelea kulipa fidia kwa wananchi wote kadiri tutakavyo pata fedha kutokana na mauzo ya viwanja.

15.5 Mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Kutokana na ufinyu wa Bajeti Wilaya imeweza kuandaa mpango wa matumizi bora ya Ardhi kwa Vijiji 12 kati ya vijiji 111 vilivyopo. Wilaya inatambua kuwa mpango wa matumizi bora ya ardhi ni njia pekee ya kuondoa migogoro mingi ya ardhi inayojitokeza baina ya wakulima na wafugaji. Wilaya itaendelea kupima na kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi wa vijiji vilivyobaki kadiri fedha itakavyokuwa inapatikana.

15.6 Migogoro ya ardhi na utatuzi wake.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Ulijitokeza mgogoro wa kijiji cha Katapulo na kampuni ya ranchi ya kalambo na ukatatuliwa na mkurugenzi wa upimaji ramani ambaye alitoa maelekezo kwa kijiji kuzingatia mipaka iliyopimwa. Pia mgogoro wa Serikali ya Kijiji cha Mao na Mwananchi mmoja, wataalam toka

ngazi ya Wilaya walifanya usuluhishi lakini pande hizo mbili hazikukubaliana kwa ufumbuzi zaidi wataalam walimshauri Mwananchi anayelalamika apeleke malalamiko yake kwenye vyombo vyaa sheria.

16 SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya kuitia sekta ya Maendeleo ya Jamii imefanikiwa kusajili vikundi vya kijamii 217. Kati ya vikundi hivyo, vikundi 11 vya wanawake na vijana vimeweza kupatiwa mkopo wenyenye jumla ya shilingi 17,144,000/= kuitia mfuko wa WDF na kikundi kimoja cha vijana kati ya hivyo kimepatiwa mkopo kutoka Wizara ya Vijana, Utamaduni na Michezo. Kati ya Vikundi hivyo 11, vikundi vine (4) vimerejesha mkopo wote mapema na vilivyobaki saba (7) bado havijarejesha mkopo wao wa kiasi cha Tshs.10,326,000/=.

16.1 Mpango wa kunusuru kaya maskini – TASAF

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo kuitia Mfuko wa TASAF awamu ya tatu katika kipindi cha Julai 2015 hadi Juni 2016 imepokea Jumla ya shilingi 1,198,188,000/=, ambapo matumizi yake ni kiasi cha shilingi 1,197,079,757.28 kuitia Mpango wa kunusuru kaya masikini. Kaya zipatazo 4,674 zimeweza kufikiwa kuitia mpango huu katika viji 66 vilivyopo kwenye mpango.

16.2 Taarifa dhidi ya mapambano ya UKIMWI

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ina wateja 1195 wa tiba na matunzo, na walio katika dawa za kupunguza makali ya VVU/UKIMWI ni 1098, na watoto chini ya miaka 5 walioko katika dawa ni 57.

Mafanikio dhidi ya maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI

- a. Mambukizi ya VVU/UKIMWI yamepungua kutoka 2.8% 2013 hadi 2.3% 2016

- b. Vituo vya upimaji wa hiari wa VVU/UKIMWI vimeongezeka kutoka 13 hadi 47
- c. Vituo vya PMCTC vimeongezeka kutoka 22 hadi 32
- d. Wilaya imepata mashine ya kupima CD4 kutoka katika shirika la WRP.

17 SEKTA YA NYUKI

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Sekta ya nyuki ina watumishi 7 akiwepo mkuu wa kitengo. Watumishi wawili wapo makao makuu ya Wilaya na watano wapo katika ngazi ya tarafa.

Eneo linalofaa kwa ufugaji nyuki kwa Wilaya ya Kalambo ni takribani hekta 37,278 ambapo kuna maji ya kutosha na hifadhi za misitu shirkishi na ile ilio chini ya uangalizi wa Serikali kuu. Jumla ya watu takribani 900 hujihusisha na shughuli za ufugaji nyuki. Wilaya ina mizinga ya kisasa 1848, na mizinga 600 ya kienyeji. Pia tuna jumla ya vikundi 40 vya wajasiliamali wanaojihusisha na shughuli za ufugaji nyuki.

Uzalishaji wa asali kwa msimu uliopita ulikua tani mbili na nusu kwa mwaka na nta iliyozalishwa ni kilo 600. Tunategemea kuvuna kiasi kikubwa cha asali msimu huu mpya baada ya ongezeko la mizinga ya kisasa ambapo mzinga mmoja unaweza kuvuna kilo 30 mpaka 40 za asali kwa msimu mmoja ukilinganisha na mizinga iliyokuwepo awali ilikua na uwezo wa kuzalisha kilo 15, mpaka 20 za asali. Wilaya imewawezesha wafugaji wawili pamoja na wataalum wawili kuhudhuria maonyesho ya nane nane Mbeya ili kuweza kujifunza zaidi namna ya ufugaji bora wa nyuki na usindikaji wa mazao ya nyuki ili kuongeza thamani ya asali na nta.

18 SEKTA YA SHERIA

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya kuitia Kitengo cha sheria imefanikiwa kutunga sheria ndogo za Halmashauri na tayari zimepitishwa na Baraza la Madiwani. Taratibu nyingine zinaendelea.

Sheria zilizotungwa ni kama zifuatazo;

- i. Sheria ndogo za (uhifadhi wa mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- ii. Sheria ndogo za (maliasili na vyanzo vya maji) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- iii. Sheria ndogo za (masoko na magulio) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- iv. Sheria ndogo za (kulinda na kuhifadhi maliasili na maji) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- v. Sheria ndogo za (ushuru wa madini ya ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- vi. Sheria ndogo za (ushuru wa huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- vii. Sheria ndogo za (uvunaji na uhifadhi wa maji ya mvua) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- viii. Sheria ndogo za (ada na ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- ix. Sheria ndogo za (bodi ya uendeshaji wa soko la samaki kasanga) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- x. Sheria ndogo za (kazi za songambele, ulinzi wa umma na ulinzi shirikishi jamii) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- xi. Sheria ndogo za (uthibiti wa uchafuzi na uharibifu wa mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- xii. Sheria ndogo za (kuthibiti omboaomba) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.

- xiii. Sheria ndogo za (masoko na magilio) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- xiv. sheria ndogo za (matumizi ya barabara) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- xv. Sheria ndogo za (maliasili na vyanzo vya maji) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- xvi. Sheria ndogo za (bodi ya mfuko wa maendeleo ya elimu) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- xvii. Sheria ndogo za (utozaji wa ada za leseni za barabara) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- xviii. Sheria ndogo za (kilimo kwanza na usalama wa chakula) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- xix. Sheria ndogo za (usafirishaji pikipiki na bajaji) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.
- xx. Sheria ndogo za (ushuru wa madini na ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya kalambo za mwaka 2016.

19 SEKTA YA TEHAMA

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ina maafisa TEHAMA wawili na kwa ujumla hali ya mifumo ya TEHAMA katika Wilaya Kalambo kwa sasa sio nzuri kutokana na sababu zifuatazo;

- a. Kutokuwepo mkongo wa Taifa.
- b. Kutokuwepo kituo cha taarifa (Server)
- c. Kutokuwepo miundombinu ya mtandao kiambó (Local Area Network-LAN) na huduma ya intaneti katika majengo ya ofisi ya za Serikali
- d. Kutokuwepo mfumo wa udhibiti matumizi ya fedha 'EPICOR'
- e. Kutokamilika mfumo wa ukusanyaji wa mapato kielektronik 'LGRCIS'

20 HALI YA UWEKEZAJI WILAYANI NA FURSA ZA UWEKEZAJI ZILIZOPO

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya imekuwa ikifanya juhudi katika kuhakikisha fursa za uwekezaji zilizopo Wilayani zinatangazwa na kuendelezwa kwa manufaa ya wananchi wa Wilaya ya Kalambo na wawekezaji wenyewe. Pamoja na kuwa Wilaya imejaliwa kuwa fursa nyingi bado Wilaya haijapata wawekezaji wa kiwango cha kuridhisha.

Jedwali Na. 25: Orodha ya fursa zilizopo katika Wilaya ya Kalambo

Na	Sekta	Fursa za Uwekezaji Wilayani	Mahali Zilipo Fursa
1	Utalii	1. Maporomoko ya Kalambo	1. Kapozwa
		2. Ziwa Tanganyika	2. Vijiji vya mwambao wa Ziwa Tanganyika
		3. Maporomoko ya Lwanji	3. Kafukoka
		4. Maporomoko ya Namkale	4. Kapozwa/Safu
		5. Chemichemi ya maji moto	5. Kizombwe
2	Uvuvi	Uvuvi	Kasanga na vijiji vya mwambao
		Ufugaji wa samaki	Katuka na Mwimbi
3	Viwanda	Usindikaji wa mazao ya samaki	Kasanga -vijiji vya mwambao
		Usindikaji wa mazao ya kilimo	Matai, Ulumi
		Usindikaji wa mazao ya mifugo	Matai
4	Nyuki	Ufugaji/usindikaji wa mazao ya nyuki	Msitu wa Kalambo
5	Biasara	Huduma za Hoteli	Matai/Kasanga/ Kasesya

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya ya Kalambo inao wawekezaji wachache waliojitokeza ambao tayari wameshawekeza kama inavyoonekana katika Jedwali.

Jedwali Na. 26: Orodha ya wawekezaji waliopo katika Wilaya ya Kalambo

Na.	Jina la Mmiliki	Kijiji	Hekari	Uwekezaji anaofanya
1	Mikebuka Fisheries Co. Ltd	Muzi	1.2	Usindikaji wa samaki
2	Bismarck Co. Ltd	Kasanga	3.5	Hoteli, Utalii na samaki wa mapambo

21 CHANGAMOTO, MIKAKATI NA UTATUZI WA CHANGAMOTO

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Wilaya inakabiliwa na changamoto mbalimbali, pia imejipanga kukabiliana na changamoto hizo kuitia mikakati mbalimbali kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo;

Na.	CHANGAMOTO	UTATUZI WA CHANGAMOTO
1	Ukosefu wa nyumba za Watumishi.	<ul style="list-style-type: none"> - Wilaya inaendelea na ujenzi wa nyumba 7 za watumishi kwa upande wa Halmashauri na nyumba 3 ofisi ya Katibu Tawala Wilaya - Aidha tunaendelea kuomba fedha katika Bajeti kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya Ujenzi wa Nyumba za watumishi.
2	Watumishi wanaidai Serikali madeni yaliyohakikiwa na Mkaguzi wa ndani wa Wilaya yenye jumla ya Tshs. 681,188,644/=	Madai yameshawasilishwa Serikali kuu ili yaweze kulipwa.
3	Ufinyu wa makusanyo ndani ya Halmashauri.	Wilaya itaendelea kuongeza wigo wa mapato pamoja kusimamia kikamilifu vyanzo vilivvopo.
4	Kukosekana kwa huduma ya Benki na vituo vya mafuta ya kuendeshea magari na mitambo.	<ul style="list-style-type: none"> - Kuna mwekezaji mmoja ambaye anaendelea na ujenzi wa kituo cha Mafuta - Benki ya NMB inaendelea kukamilisha miundombinu ya kibenki katika Ofisi za Halmashauri, tunatarajia huduma hii kuanza kutolewa hivi karibuni.
5	Fedha za Ruzuku ya OC na za Maendeleo zilizoidhinisha katika Bajeti kutofika kwa wakati na wakati mwingine kutofika kabisa.	Kuendelea kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato ya ndani ili shughuli za utoaji wa huduma kwa wananchi zisikwame

Na.	CHANGAMOTO	UTATUZI WA CHANGAMOTO
6	Kukosekana kwa Hospitali ya Wilaya.	<ul style="list-style-type: none"> - Kwanza tutaendelea kuboresha kituo cha Afya Matai ili kiweze kutoa huduma kikamilifu. - Pili, tutaendelea kutenga fedha katika Bajeti kwa ajili ya Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.
7	Upungufu mkumbwa wa madarasa, vyoo na nyumba za watumishi shuleni.	Wilaya inaendelea kuhamasisha wadau wa maendeleo na wananchi katika kuboresha miundombinu kwa kupitia vikao vya kamati/bodi za shule na Serikali za vijiji/Kata na kuiomba serikali kupitia bajeti za kila mwaka kwa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya madarasa, vyoo na nyumba za watumishi.
8	Ongezeko kubwa la mifugo (Ng'ombe) katika Wilaya ya Kalambo. Kumekuwepo na ongezeko kubwa la mifugo katika Wilaya lisiloendana na ukubwa wa eneo la malisho kutokana na baadhi ya wafugaji kuingiza mifugo yao ndani ya Wilaya bila ya kufuata taratibu hivyo kupelekea uwepo wa migogoro ya wafugaji na wakulima katika baadhi ya maeneo.	<ul style="list-style-type: none"> - Viongozi ngazi ya Kata na Vijiji wamepewa Muongozo unaotakiwa katika kumruhusu mfugaji kuhamishia mifugo ya kufuga kutoka sehemu moja kwenda nyingine. - Mkuu wa Wilaya alifanya mikutano mbalimbali katika kata za legezamwendo na Mambwenkoswe juu ya suala la mifugo.

22 HITIMISHO

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Tunaendelea kukushukuru kwa kuja kututembelea katika Wilaya yetu ya Kalambo na tunaendelea kukutakia kila la heri na Baraka tele za Mwenyezi Mungu katika ziara yako Wilayani kwetu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Naomba kuwasilisha.

**Julieth N. Binyura
MKUU WA WILAYA
WILAYA YA KALAMBO.**